MTAALA WA UMILISI

G4

Muda: Saa 1 dakika 40

MIDTERM

SEHEMU YA KWANZA: KISWAHILI - LUGHA

Soma kifungu hiki kisha ujibu swali la 1 -5.



Mazingira yetu lazima yawe safi.Tunafaa kupanda miti mingi.Miti huleta hewa safi na mvua.Tunapata matunda kutokana na miti.Tusiharibu maji ya mito na mifereji. Mazingira machafu huleta afya mbaya. Nzi na mbu huleta magonjwa. Mbu huleta ugonjwa wa malaria na nzi huleta ugonjwa wa kipindupindu.

Tuweke mazingira yetu safi ili tusipate magonjwa.Tunaweza kuweka mazingira yetu safi kwa njia mbalimbali.Tumia choo unapoenda haja.Tupa taka kwenye pipa kisha uzichome.Tusichafue mito kwa uchafu, tufagie tunapoishi na mwisho tusikate ~~miti ovyo.~~

Maswali

1. Miti haileti_____
   A. matunda
   B. hewa safi
   C. mchanga
   D. mvua.

2. Afya mbaya huletwa na_____
   A. mvua
   B. nzi
   C. mbu
   D. mazingira machafu.

3. Mdudu aletaye ugonjwa wa kipindupindu huitwa_____
   A. nzi
   B. inzi
   C. umbu
   D. mbu.